JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA

IMEIDHINISHWA KWA KIWANGO CHA ISO 9001:2015

## TAARIFA KWA UMMA

# TCAA YAIMARISHA MAANDALIZI DHIDI YA ATHARI ZINAZOWEZA KUSABABISHWA NA EL NIÑO

Kufuatia maelekezo ya Serikali kuhusu maandalizi dhidi ya athari zinazoweza kusababishwa na El Niño, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imeendelea kuimarisha hatua za kuhakikisha kuwa sekta ya usafiri wa anga inajiandaa ipasavyo kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza.

Hatua hizo zinafuatia tahadhari iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) tarehe 18 Agosti 2026 kuhusu uwezekano wa athari za El Niño kwa mwaka 2026. Tahadhari hiyo inaonesha uwezekano mkubwa wa kutokea kwa hali mbaya ya hewa, ikiwemo mvua kubwa, mafuriko, upepo mkali na ngurumo za radi.

Hali hizo zinaweza kuathiri shughuli za viwanja vya ndege, upatikanaji wa umeme, mifumo ya mawasiliano, miundombinu ya barabara na huduma nyingine muhimu zinazowezesha shughuli za usafiri wa anga. Kwa hiyo, maandalizi ya mapema na uratibu madhubuti ni muhimu ili kulinda usalama wa anga na kuhakikisha mwendelezo wa shughuli.

TCAA inatoa wito kwa mashirika ya ndege, wamiliki wa viwanja vya ndege, watoa huduma za uongozaji ndege, watoa huduma wengine za usafiri wa anga, watumishi na wadau husika kupitia na kuimarisha mipango yao ya kukabiliana na dharura, mwendelezo wa shughuli na tahadhari. Wadau wanahimizwa kufuatilia kwa karibu utabiri na tahadhari rasmi za hali ya hewa zinazotolewa na TMA, na kuchukua hatua kwa wakati ili kulinda miundombinu muhimu na mifumo ya uendesha¡i.

Mamlaka itaendelea kufuatilia utabiri, tahadhari na taarifa nyingine muhimu zinazotolewa na TMA na kutoa taarifa na mwongozo unaofaa kadiri taarifa zaidi zitakavyopatikana.

**Imetolewa tarehe 11 Septemba 2026.**



Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Fri Sep 11 17:38:19 EAT 2026

Dr. Jabiri K. Bakari
**Mkurugenzi Mkuu**

Aviation House, Mwisho wa Barabara Nyerere/Kitunda, S.L.P 2819, Dar es Salaam, Tanzania
Email: dg@tcaa.go.tz Telephone: +255-282 560333